JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barua pepe: rbcsingida@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAKUKURU Mkoa,
S. L. P 484,
43108 Singida.

TAARIFA KWA UMMA

Singida
Oktoba 27, 2023

TAKUKURU SINGIDA YAOKOA SHS. 54,087,750.58 ZILITOKANA NA WAZABUNI KUTOWASILISHA KODI YA ZUIO TRA na KUPELEKA VIFAA PUNGUFU KATIKA MIRADI TOFAUTI.

Ndugu Wanahabari,

1. UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU Mkoa wa Singida kwa kipindi cha Julai – Septemba 2023 kwa upande wa **UZUIAJI RUSHWA** tumefuatilia utekelezaji wa miradi **Kumi na tatu (13)** yenye thamani ya zaidi shilingi bilioni tano **(5,627,138,826)** katika sekta ya Elimu na Barabara.

Hii inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na fedha za Serikali Kuu zilizoelekezwa Mkoa wa Singida kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Miradi mitatu **(3)** iliyofuatiliwa yenye thamani ya **Sh. 1,480,200,000/=** ilikutwa na mapungufu mbalimbali na ushauri ulitolewa ili kukabiliana na mapungufu hayo. (**Rejea kiambatisho Na. 1)**

Kutokana na ufuatiliaji wa miradi uliofanyika, ofisi ilifanikiwa kuokoa fedha Sh. **54,087,750.58** zilitokana na kutowasilishwa kwa kodi ya zuio TRA na wazabuni kupeleka vifaa pungufu katika miradi tofauti na madai aliyowasilisha au fedha alizolipwa**. (Rejea kiambatisho Na. 2).**

1.1 CHAMBUZI ZA MIFUMO

TAKUKURU Mkoa wa Singida katika kipindi tajwa ilifanya **chambuzi saba** za mifumo ili kubaini mianya ya rushwa iliyopo katika maeneo hayo na kisha kushauri namna ya kuiziba (**Rejea kiambatisho Na. 3).**

Warsha saba (7) zilifanyika za kujadili mianya ya rushwa iliyobainika katika chambuzi zilizofanyika na kuweka mikakati ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika. (**Rejea kiambatisho Na. 3).**

Ndugu Wanahabari,

Ofisi iliendelea na utekelezaji wa **Programu ya TAKUKURU RAFIKI** kwa kufanya vikao **18** na wadau katika kata **18** ambapo wadau waliibua kero **175**. Kero zilizotatuliwa mpaka sasa ni **125** na kero 50 zinaendelea kupatiwa ufumbuzi. **(Kiambatisho Na. 4).**

2. ELIMU KWA UMMA

Kwa upande wa Elimu kwa Umma, ofisi iliwaongezea wananchi uelewa wa masuala ya rushwa kwa kufanya; Semina **34** kwenye makundi mbalimbali wakiwemo watumishi wa umma. Pia tulifanya mikutano ya hadhara **17**, maonesho 7, kutembelea na kuimarisha klabu za wapinga rushwa **43** katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. (**Rejea kiambatisho Na. 5).**

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Malalamiko **76** yalipokelewa, ambapo malalamiko 52 yalihusu vitendo vya rushwa na malalamiko 24 hayakuhusu rushwa. Malalamiko **52** yaliyohusu rushwa uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na malalamiko **24** ambayo hayahusiani na rushwa walalamikaji walipewa ushauri. **(Rejea kiambatisho Na. 6 na Na. 7).**

Katika kipindi tajwa kesi 10 zilifunguliwa mahakamani, kesi 13 ziliamuliwa, kesi 8 zilishinda. (**Rejea kiambatisho Na. 8).**

TAKUKURU (M) Singida kwa robo ya pili ya mwaka 2023/2024 ya kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2023 imeweka Mkakati wa utendaji kazi kwa kufanya yafuatayo;

1. kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali zinazoelekezwa Mkoa wa Singida kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

2. Kuendelea kuwaongezea uelewa wananchi kuhusiana na masuala ya rushwa ili wananchi washiriki kikamilifu katika kuzuia vitendo hivyo hasa katika miradi ya maendeleo inayoendelea katika maeneo yao.
3. Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU – Rafiki.

WITO:

TAKUKURU (M) wa Singida inatoa RAI kwa wananchi wote kujiepusha na vitendo vya rushwa na kushiriki kikamilifu kuzuia vitendo vya rushwa vinavyotokea katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii. Pia, kuzuia vitendo hivyo hasa katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao, na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa njia zifuatazo:

i. Kufika Ofisi za TAKUKURU (M) Singida na Wilaya za Iramba, Ikungi, Mkalama na Manyoni.

ii. Kupiga simu ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa na wakuu wa TAKUKURU wa Wilaya kwa namba zifuatazo:

Na	Mkoa /Wilaya	NAMBA YA SIMU
1	RBC –Singida	0738150208
2	DBC - Mkalama	0738150 212
3	DBC - Ikungi	0738150213
4	DBC - Iramba	0738150 210
5	DBC - Manyoni	0738150 211

iii. Kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi na kushiriki kutoa ushahidi Mahakamani.

KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU

Imetolewa na:

MKUU WA TAASISI (M)
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA
NA RUSHWA
(TAKUKURU)
MKOA WA SINGIDA

SIPHA MWANJALA
KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) SINGIDA
SIMU: 0738150208